



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA



Tovuti: www.hpc.go.tz

TANGAZO

KUFUNGUA DIRISHA LA MAOMBI YA UTARAJALI

Baraza la Wataalam wa Maabara linachukua nafasi hii kuwajulisha wahitimu wote wa shahada ya maabara ya afya Binadamu kuwa dirisha la maombi ya utarajali litafunguliwa tarehe **17.10.2023** Saa 4:00 Ashuhuhi. Aidha; dirisha litafungwa tarehe **18.10.2023** saa 9:30 alasiri. Maombi yote yatafanyika kuitia mfumo wa **hprs.moh.go.tz**

Mambo Muhimu ya kuzingatia;

1. Wahitimu wanaoruhusiwa kufanya maombi ya utarajali ni wale tu ambao wamefaulu na kupata barua ya utambulisho kutoka chuoni.
2. Wahitimu waliosoma vyuo vya nje ya nchi wanatakiwa kuhakikisha wameambatanisha barua ya uthibitisho kutoka TCU pamoja na cheti cha matokeo au cha Chuo.
3. Waombaji wote wanatakiwa wawe wamefanya maombi ya usajili wa awali na usajili huo uwe umeithinishwa (Approved).
4. Waombaji wote wanasisitizwa kufanya maombi kwa wakati na kama atahitaji kubadilisha kituo cha utarajali atafanya hivyo kwa kituo chenye nafasi kabla dirisha halijafungwa. Baada ya dirisha kufungwa hakutakuwepo na uwezekano wa kubadili kituo cha utarajali.

Aidha; Wale wote watakaopangiwa vituo vya utarajali wanatakiwa kufika Dodoma tarehe **27.10.2023** saa 2:00 Asubuhi kwa ajili ya kupata maelekezo pamoja na nyaraka za kipindi cha utarajali. Kikao hiki kitafanyika katika Chuo kikuu cha Dodoma, Kitivo cha Tiba. Siku ya hiki kikao wote wafike na barua za utambulisho pamoja, waliosoma vyuo vya nje wafike na uthibitisho (Recognition award) kutoka TCU

Ofisi ya Msajili inawatakia utekelezaji mwema.

Kwa maeleo zaidi piga simu 0734005777

Imetolewa na:

Ofisi ya Msajili

Baraza la Wataalam wa Maabara.

12.10.2023

